

# PRECISION LIVESTOCK FARMING TECHNOLOGIES EVALUATION

## MASWALI YANAYOULIZWA MARA KWA MARA (FAQ )

### Utafiti wa matumizi ya teknolojia ya CERES tags katika ng'ombe wa nyama

#### Q1. CERES TAG NI NINI NA INAKAA SEHEMU GANI YA NG'OMBE?

Hiki ni kifaa ambacho ng'ombe anavaa kama hereni na kinakaa juu ya sikio la mnyama, kama inavyoonyesha kwenye picha.



#### Q2. MFUMO WA HIZI HERENI AINA YA CERES UNAFANYAJE KAZI?

CERES ni suluhisho kamili la ufuatiliaji inayotumia teknolojia ya mfumo wa dunia wa kisatelaiti (GPS) kufuatilia mifugo yako. Kifaa hiki hutuma data moja kwa moja kwenye satelaiti na kuweza kuzipata kupitia simu yako.

#### Q3. JE, HIZI HERENI ZITAKUWA NA MANUFAA GANI KWANGU KAMA MFUGAJI?

Hereni hizi zinatoa taarifa mbalimbali juu ya mifugo yako, mfano, itakujulisha mwenendo wa wanyama wako katika ulaji, unywaji wa maji, umbali gani ng'ombe ametembea, na mabadiliko mengine ya mwili. Taarifa hizi zitakusaidia kufanya maamuzi sahihi na kwa wakati kuhusu usimamizi wa mifugo yako.

#### Q4. NIFANYE NINI IKIWA HERENI ITAANGUKA AU IKIWA MNYAMA WANGU ATAPOTEA?

Kifaa kinaweza kufuatiliwa kwa kutumia teknolojia ya satelaiti. Hii itawezesha ufuatiliaji endelevu na urejeshaji wa hereni au mnyama.

#### Q5. JE, KUVAA HERENI KUNAWEZA KUMDHURU NG'OMBE?

Hapana, hereni imeundwa kuwa nyepesi na isiyoingilia shughuli za kawaida za ng'ombe, na haiwezi kumdhuru au kumsumbua ng'ombe.

#### Q6. MAAFISA UGANI WATAWAZAJE TAARIFA WAKATI NG'OMBE WANAPOENDA MAENEO YA MBALI KWA AJILI YA MALISHO?

Maafisa ugani wataweza kufuatilia mahali halisi walipo ng'ombe kupitia mfumo. Pia utajulishwa mahali walipo.

#### Q7. NITAPOKEAJE TAARIFA KUHUSU WANYAMA WANGU?

Utapokea taarifa kwa njia ya meseji kwenye simu yako (SMS) kila siku, zenye taarifa ya kila ng'ombe aliyefungwa hereni ikionesha taarifa za ulaji wa mnyama, muda aliotumia kutembea, kula au kunywa maji.

#### Q8. JE, KUNA ADA YOYOTE INAYOHUSIANA NA HUDUMA HII?

Hapana, hutatozwa ada kwa huduma hii kwani mradi ndiyo unawajibika.

# MASWALI YANAYOULIZWA MARA KWA MARA (FAQ )

## Q9. ITAKUWAJE NIKITAKA KUUZA NG'OMBE ALIYEWEKWA HERENI?

Inashauriwa kuweka hereni kwa ng'ombe ambao hupangi kuuza kwa angalau miaka miwili ijayo. Hata hivyo, ikiwa hali itabadilika na utaamua kuuza ng'ombe aliyewekwa hereni, tafadhali mjulishe afisa ugani mapema.

## Q10. NINI KITAFANYIKA KAMA NG'OMBE AKIFA AKIWA NA HERENI?

Tunatumaini ng'ombe wote wataendelea kuwa na afya njema, lakini kwa bahati mbaya ng'ombe akifa, tafadhali mjulishe afisa ugani.

## Q11. TAYARI TUNAJUA WAKATI WA KUHAMISHA NG'OMBE KWENDA KWENYE MALISHO BORA ZAIDI. UTAFITI HUU UTATUNUFAISHAJE?

Utafiti huu unalenga kutoa uelewa wa kina zaidi juu ya aina au mahali maalum pa nyanda za malisho yanayopendwa na ng'ombe wako na ubora wa malisho hayo. Maarifa haya yataweza kuunga mkono mapendekezo ya sera, kama vile kuhimiza kupanda nyasi zinazostahimili ukame, ambazo zinaweza kupunguza haja ya kuwapeleka ng'ombe umbali mrefu.

## Q12. JE, HERENI ZA NG'OMBE ZITAWEKWA LINI?

Afisa ugani anayehusika na eneo lako atakujulisha kuhusu ratiba ya kuweka hereni.

## Q13. JE, NI LAZIMA KUWEKA HERENI KWA KILA NG'OMBE KATIKA KUNDI LANGU?

Hapana, si lazima kuweka hereni kwa kila ng'ombe. Utafiti huu unapendekeza kuweka hereni kwa ng'ombe wanne tu.

## Q14. JE, HERENI INAJUAJE KIASI GANI CHA MALISHO AMBACHO NG'OMBE AMEKULA?

Kupitia taarifa muhimu kama vile muda ambao ng'ombe ametumia kula. Taarifa hizi zinaungwa mkono na miaka 15 ya utafiti na majaribio ya kina, kuhakikisha matokeo ya kuaminika.

## Q15. JE UKILINGANISHA NA UZOEFU WANGU WA USIMAMIZI WA MIFUGO, TAARIFA HIZI ZITANISAIDI NINI?

Taarifa itasaidia kumjua ng'ombe mmoja mmoja na kundi zima. Kwa kuchambua mwenendo wa kila siku na kila wiki, unaweza kutambua mabadiliko ya tabia na kufanya maamuzi kwa wakati sahihi ili kuboresha uzalishaji na afya ya kundi lako kwa ujumla.

## Q16. JE, NI MATENGENEZO GANI YANAYOHITAJIKA KWA HERENI?

Hereni hizi hazihitaji matengenezo, zimetengenezwa kwa ajili ya matengenezo madogo sana. Ila utakuwa ukiikagua hereni ya kila ng'ombe mara kwa mara, ili kubaini kama ipo salama.

## Q17. JE, HIZI HERENI HUDUMU KWA MUDA GANI KABLA YA KUHITAJI KUBADILISHWA?

Hereni imeundwa kuwa imara na hudumu kwa miaka mitatu, kulingana na hali na jinsi unavyozitunza.

## Q18. NINI KITAFANYIKA IKIWA HERENI ITAHARIBIKA AU KUACHA KUFANYA KAZI?

Ikiwa hereni itaharibika au kuacha kufanya kazi, tafadhali wasiliana na afisa ugani mara moja. Watawasaidia kutatua tatizo husika.

## Q19. JE, USALAMA WA TAARIFA ZITAKAZOKUSANYWA UPOJE?

Taarifa zitakazo kusanywa zitahifadhiwa kwa usalama na zitatumika tu kwa ajili ya utafiti.